



## Adhkari zinazo semwa asubuhi na jioni

Ameandika Muhammad Swalehe  
Al-Uthaymini Tarehe: 1418-1-20 H

## الإسلام بأكثر من 100 لغة



رقم الإيداع:



Sw312 - t3

«لا إله إلا الله وحده لا شريك له. له الملك وله الحمد. وهو على كل

شيء قدير» (مائة مرة) في الصباح أو المساء

“Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, Mwenye ufalme na Mwenye sifa na yeye juu ya kila kitu ni Muweza.”

(mara mia moja) asubuhi na jioni.

«حسبى الله لا إله إلا هو عليه توكلت وهو رب العرش العظيم» (سبع مرات)

“Ananitoshia Allah hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye na Yeye ni Mmiliki wa Arshi (kiti cha enzi) kitukufu.” (mara saba).

«سبحان الله وبحمده»

(مائة مرة) في الصباح أو المساء، أو فيهما جميعًا

“Utakasifu ni wa Allah na Sifa njema ni zake”

(mara mia moja) Asubuhi na jioni. Au nyakati zote kwa pamoja.

«أستغفر الله وأتوب إليه» (مائة مرة)

“Ninamtaka Mwenyezi Mungu msamaha na ninatubia kwake.” (mara mia moja).

Haya ndiyo yaliyo wezekana kuyaandika, nina muomba Allah Mtukufu anufaishe kwayo umma.

## Adhkari zinazosemwa asubuhi na jioni

Ameandika Muhammad Swalehe  
Al-Uthaymini Tarehe: 1418-1-20 H

على. وأبوء بذنبي. فاغفر لي. فإنه لا يغفر الذنوب إلا أنت»

“Ewe Mwenyezi Mungu wewe ndiye Mola Mlezi hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, umeniumba na mimi ni mja wako na mimi nipo juu ya ahadi yako na maonyo yako kwa kiasi niwezavyo, ninataka hifadhi kwako kutokana na shari niliyo ifanya, ninakiri kwa neema zako zilizo juu yangu, na ninakiri kwa madhambi yangu, basi nisamehe mimi, kwani hakuna afutae madhambi isipokuwa wewe.”

«اللهم فاطر السماوات والأرض. عالم الغيب والشهادة. رب كل شيء ومليكه. أشهد أن لا إله إلا أنت. أعوذ بك من شر نفسي ومن شر الشيطان وشركه وأن أقترف على نفسي سوءاً أو أجره إلى مسلم»

“Ewe Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi, mjuzi wa yaliyofichikana na yenye kuonekana, Mola Mlezi wa kila kitu na mmiliki wake, ninakubali ya kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, ninajikinga kwako kutokana na shari za nafsi yangu na kutokana na shari za shetani namitego yake, na ninajikinga kwako kuto fanya juu ya nafsi yangu ubaya au nikaupeleka kwa muislamu.”

«اللهم إني أصبحت أشهدك وأشهد حملة عرشك وملائكتك وأنبياءك وجميع خلقك بأنك أنت الله لا إله إلا أنت وأن محمداً عبدك ورسولك» (أربع مرات)

“Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nimepambazukiwa na asubuhi, ninakufanya Wewe kuwa shahidi na ninawashuhudisha Malaika wabebao Arshi yako na Malaika wako kwa ujumla na Manabii wako na viumbe wako wote kuwa wewe ni Allah, hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe na kuwa Muhammad ni mja wako na Mtume wako.”

«اللهم إني أمسيت...»

Na jioni Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nimeingia jioni...Mpaka mwisho (mara nne)

# Adhkari zinazo semwa asubuhi na jioni

Ameandika Muhammad Swalehe  
Al-Uthaymini Tarehe: 1418-1-20 H

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.

﴿اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ﴾ البقرة: 255

﴿Mwenyezi Mungu hakuna mola isipokuwa Yeye,(na) ndiye Mwenye uhai wa maisha, Msimamia kila jambo, Kusinzia hakumshiki wala kulala. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake (Mungu) bila idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, hawalijui lolote katika elimu Yake (Mwenyezi Mungu) isipokuwa kwa alipendalo (Mwenyezi Mungu).Kiti chake cha Enzi kimeenea mbingu na na ardhi, wala kuvilinda hivyo hakumshindi, na Yeye (peke yake) ndiye aliye juu na ndiye aliye Mkuu﴾

Ayatul Kursiy 255 Al Baqarah.

﴿عَامَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نَفَرَقَ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ﴾ لَا يَكْفُلُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ رَبَّنَا لَا

تُؤَاخِذُنَا إِنْ نَسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلَا تُحِثْ عَلَيْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ وَاعْفُ عَنَّا وَاعْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا أَنْتَ مَوْلَانَا فَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ﴾ البقرة: 285-286.

﴿Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na Waislamu, (pia wameamini hivyo) wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na vitabu vyake, na Mitume wake hatutofautishi baina ya yeyote katika Mitume wake, na husema tumesikia na tumetii (Tunakuomba msamaha Mola wetu na marejeo ni kwako\*Mwenyezi Mungu hailazimishi nafsi yoyote isipokuwa yaliyo sawa na uweza wake. (Faida ya) yale iliyochuma (nafsi hiyo) ni yake na hasara ya yale iliyochuma ni juu yake. (Husema); Mola wetu usitutese kama tukisahau au tukikosa, Mola wetu na usitubebeshe mzigo kama uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu usitutwike tusingoyaweza na utusamehe na utufutie na uturehemu, Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tusaide juu ya watu makafiri.﴾

Aya 285-286.Al Baqarah

﴿قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ﴾ الإخلاص: 1.

﴿Sema ni Yeye Mwenyezi Mungu Mmoja.﴾

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْقَلْقِ﴾ الفلق: 1.

﴿Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko.﴾

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ﴾ الناس: 1.

﴿Sema: Ninajikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu.﴾

(السورة كاملة ثلاث مرات) ..... Zitasomwa sura zote tatu kwa ukamilifu mara tatu tatu.

﴿أعوذ بكلمات الله التامات من شر ما خلق﴾ (ثلاث مرات)

﴿Ninajikinga kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyo timia kutokana na shari alizo ziumba.﴾ Mara tatu.

﴿بِسْمِ اللَّهِ الَّذِي لَا يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّوْمِيُّ الْعَلِيمُ﴾ (ثلاث مرات)

﴿Kwa jina la Mwenyezi Mungu ambaye hakidhuru kitu chochote (kwa kutaja) pamoja na jina lake (Mwenyezi Mungu) katika ardhi wala katika mbingu na Yeye ni Mwenye kusikia Mwenye ujuzi.﴾ Mara tatu.

﴿رضيت بالله رباً وبالإسلام ديناً وبمحمد صلى الله عليه وسلم نبياً﴾ (ثلاث مرات)

﴿Nimeridhia kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Mola Mlezi na uislamu ndio dini ya kweli na Muhammadi-Rehema na amani ziwe juu yake ni Nabii.﴾ Mara tatu.

﴿أصبحنا وأصبح الملك لله والحمد لله لا إله إلا الله وحده لا شريك له. له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير. رب أسألك خير ما في هذا اليوم وخير ما بعده. وأعوذ بك من شر ما في هذا اليوم ومن شر ما بعده. رب أعوذ بك من الكسل والههم وسوء الكبر. وأعوذ بك من عذاب النار وعذاب القبر﴾

﴿Tumeingia asubuhi na ufalme wa asubuhi umethibiti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake, Ufalme ni wake na sifa ni zake na Yeye juu ya kila kitu ni Muweza,Ewe Mola Mlezi ninakuomba heri zinazo patikana ndani ya siku hii na heri za baada ya siku hii, na ninajikinga kwako kutokana na shari za siku hii na shari za baada ya siku hii,Ewe Mola Mlezi ninajikinga kwako kutokana na uvivu na uzee (ukongwe) na utu uzima mbaya, na ninajikinga kwako kutokana na adhabu ya moto na adhabu ya kaburi.﴾

﴿أمسينا وأمسى الملك لله﴾

﴿Na jioni atasema:Tumeingia jioni na ufalme wajioni umethibiti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,Na atasema:Ewe Mola Mlezi ninakuomba heri za usiku huu.Mpaka mwisho, badala ya: (tumeingia asubuhi na umethibiti) na kuhusu (siku hii).﴾

﴿اللهم بك أصبحنا وبك أمسينا وبك نحيا وبك نموت واليك النشور﴾

﴿Ewe Mwenyezi Mungu kwa ajili yako tumeingia asubuhi﴾

na kwa ajili yako tumeingia usiku na kwa ajili yako tunapata uhai na kwa ajili yako tunakufa na kwako ndiko kuna kukusanywa﴾

﴿اللهم بك أمسينا وبك أصبحنا وبك نموت وبك نحيا واليك المصير﴾

﴿Na jioni atasema:Ewe Mwenyezi Mungu kwa ajili yako tumeingia jioni na kwa ajili yako tumeingia asubuhi na kwa ajili yako tunakufa na kwa ajili yako tunapata uhai na kwako ndiko kuna kukusanywa.﴾

﴿اللهم ما أصبح بي من نعمة أو بأحد من خلقك فمنك وحدك لا شريك لك فلك الحمد ولك الشكر﴾

﴿Ewe Mwenyezi Mungu haijapambazuka kwangu au kwa yeyote katika viumbe wako neema yoyote, isipokuwa inatoka kwako peke yako hauna mshirika, basi sifa njema na shukurani ni zako﴾

﴿ما أمسى بي﴾

Na jioni atasema:Kila kilicho fikiwa na jioni kwangu ...

﴿اللهم إني أسألك العافية في الدنيا والآخرة. اللهم إني أسألك العفو والعافية في ديني ودنياي وأهلي ومالي. اللهم استر عوراتي وآمن روعاتي. اللهم احفظني من بين يدي ومن خلفي وعن يميني وعن شمالي ومن فوقي. وأعوذ بعظمتك أن أغتال من تحتي﴾

﴿Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba afya duniani na akhera, Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba msamaha na afya katika dini yangu na dunia yangu na watu wangu na mali zangu, Ewe Mwenyezi Mungu sitiri aibu zangu na unipe amani kutokana na uoga wangu, Ewe Mwenyezi Mungu nihifadhi mimi mbele yangu na nyuma yangu na kuliani kwangu na kushotoni kwangu na juu yangu, na ninajikinga kwa utukufu wako nisishambuliwe chini yangu.﴾

﴿اللهم أنت ربى لا إله إلا أنت. خلقتنى وأنا عبدك. وأنا على عهدك ووعدك ما استطعت. أعوذ بك من شر ما صنعت. أبوء لك بنعمتك﴾